**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**

# WIZARA YA KILIMO

# BODI YA KOROSHO TANZANIA

**MWONGOZO WA USAMBAZAJI WA PEMBEJEO ZA RUZUKU KWA WAKULIMA WA KOROSHO NCHINI MSIMU WA MWAKA 2025/2026**

***Mwongozo huu umetolewa chini ya Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009 na Kanuni zake za Mwaka 2010***

**Umetayarishwa na:-**

Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu,
Bodi ya Korosho Tanzania,
S. L. P 533,
**MTWARA.**

**Aprili, 2025**

## YALIYOMO

TAFSIRI YA BAADHI YA VIFUPISHO VYA MANENO YALIYOTUMIKA .................................. ii

DIBAJI ........................................................................................................................ iii

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................................ 1

2.0 MWENENDO WA USAMBAZAJI WA PEMBEJEO NA UZALISHAJI............................. 1

3.0 MADHUMUNI YA MWONGOZO............................................................................ 2

4.0 MBINU ZILIZOTUMIKA KUTAYARISHA MWONGOZO............................................ 2

5.0 MNYORORO WA USAMBAZAJI WA PEMBEJEO ZA RUZUKU ZA ZAO LA KOROSHO NCHINI ........................................................................................................ 3

6.0 UDHIBITI WA UBORA WA PEMBEJEO ................................................................ 3

7.0 GHALA KUU ZA PEMBEJEO ................................................................................ 4

8.0 USAFIRISHAJI WA PEMBEJEO ........................................................................... 4

9.0 MFUMO WA KIDIJITALI WA UGAWAJI WA PEMBEJEO.......................................... 4

10.0 USAJILI WA VITUO VYA KUGAWA PEMBEJEO..................................................... 4

10.1. UTARATIBU WA UGAWAJI WA PEMBEJEO ........................................................ 5

10.2. Usajili/Uhuishaji wa Kanzidata ya Wakulima wa Korosho ...................................... 5

10.3. Mgao na Ugawaji wa Pembejeo kwa Wakulima .................................................... 5

11.0 JINSI USAMBAZAJI NA UGAWAJI WA PEMBEJEO ULIVYO..................................... 6

12.0 UTOAJI WA ADHABU.......................................................................................... 6

13.0 USIMAMIZI, UFUATILIAJI NA TATHMINI ............................................................. 6

13.1. Muundo wa Kikosi Kazi Mkoa.............................................................................. 7

13.2. Muundo wa Kikosi Kazi Wilaya ............................................................................ 7

13.3. Muundo wa Kikosi Kazi Kata ............................................................................... 7

13.4. Sekretarieti ya Ugawaji wa Pembejeo ngazi ya AMCOS........................................ 7

14.0 UGHARAMIAJI WA VIKOSI KAZI.......................................................................... 7

15.0 GHARAMA ZA USAFIRISHAJI WA PEMBEJEO...................................................... 7

16.0 UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO ............................ 7

17.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU.............................................................................. 7

17.1. Wizara ya Kilimo ................................................................................................. 7

17.2. Kikosi Kazi cha Mkoa........................................................................................... 8

17.3. Kikosi Kazi cha Wilaya ........................................................................................ 8

17.4. Kikosi Kazi cha Kata............................................................................................ 8

17.5. Sekretarieti ya Ugawaji wa Pembejeo Kata .................... 9
17.6. Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania .................... 9
17.7. Bodi ya Korosho Tanzania .................... 10
17.8. Vyama Vikuu vya Ushirika .................... 10
17.9. Vyama vya Ushirika vya Msingi - AMCOS .................... 11
17.10. TARI Naliendele .................... 11
17.11. Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania – TFRA .................... 11
17.12. KCJEL Ltd .................... 11
17.13. Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania .................... 12
17.14. Wazabuni wa Pembejeo .................... 12
17.15. Mkulima wa Zao la Korosho .................... 12
17.16. Taasisi za Fedha .................... 13
17.17. Waandishi wa Habari .................... 13
18.0 WAJIBU WA PAMOJA .................... 13
19.0 MUDA WA UTEKELEZAJI .................... 13
20.0 ILANI .................... 13
21.0 HITIMISHO .................... 13

## TAFSIRI YA BAADHI YA VIFUPISHO VYA MANENO YALIYOTUMIKA

Katika Mwongozo huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| **"CORECU Ltd"** | Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Mkoa wa Pwani *(Coast Region Cooperative Union Limited)*. |
| **"KCJE Ltd"** | Mradi wa Pamoja ujulikanao kwa jina la *Korosho Cooperative Joint Enterprise Limited (KCJEL)* ulioanzishwa na Vyama Vikuu vya Ushirika ambavyo ni MAMCU Ltd, TANECU Ltd, TAMCU Ltd, CORECU Ltd, RUNALI Ltd na LMCU Ltd kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo, mabomba na magunia na kusambaza kwa wakulima nchini. |
| **"LMCU Ltd"** | Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya za Lindi na Kilwa *(Lindi Mwambao Cooperative Union Limited)* kutoka Mkoa wa Lindi. |
| **"MAMCU Ltd"** | Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya za Mtwara, Masasi na Nanyumbu *(Masasi Mtwara Cooperative Union Limited)* kutoka Mkoa wa Mtwara. |
| **"Mwongozo"** | Mwongozo wa usambazaji wa pembejeo, magunia na mabomba katika zao la korosho nchini kwa msimu wa mwaka 2025/2026 unaotolewa chini ya Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009 na Kanuni zake za Mwaka 2010. |
| **"RUNALI Ltd"** | Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale *(Ruangwa Nachingwea and Liwale Cooperative Union Limited)* kutoka Mkoa wa Lindi. |
| **"Sheria"** | Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009. |
| **"TACACU Ltd"** | Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Mkoa wa Tanga *(Tanga Cashewnut Cooperative Union Limited)*. |
| **"TAMCU Ltd"** | Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya ya Tunduru *(Tunduru Agricultural Marketing Cooperative Union Limited)* Mkoa wa Ruvuma. |
| **"TANECU Ltd"** | Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya za Tandahimba na Newala *(Tandahimba and Newala Cooperative Union Limited)* kutoka Mkoa wa Mtwara. |
| **"TPHPA"** | Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania *(Tanzania Plant Health and Pesticides Authority)*. |

| | |
|---|---|
| **"Wazabuni"** | Makampuni yaliyoshinda zabuni ya kusambaza pembejeo, magunia na mabomba nchini ambayo yamefunga mkataba na KCJE Ltd kwa ajili hiyo. |
| **"CBT"** | Bodi ya Korosho Tanzania *(Cashewnut Board of Tanzania)*. |

## DIBAJI

Zao la korosho ni miongoni mwa mazao ya mkakati hapa nchini yanayoliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni. Kwa mujibu wa ripoti zinazotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT); mwaka 2022/2023 korosho ililiingizia Taifa Dola za Marekani Milioni 181, mwaka 2023/2024 Dola za Marekani Milioni 221 na mwaka 2024/2025 Dola za Marekani Milioni 584. Kwa kuzingatia umuhimu huu, katika msimu wa mwaka 2025/2026, Serikali imepanga kuendelea kutoa ruzuku ya asilimia 100 kwa viuatilifu vitakavyosambazwa na Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Ushirika (KCJEL) na ruzuku ya asilimia 50 kwa upande wa mabomba. Lengo la mpango huo ni kuongeza tija na uzalishaji wa korosho ghafi na hatimaye kuleta manufaa ya kipato kwa wakulima na Taifa kwa ujumla.

Utayarishaji wa mwongozo huu umejumuisha maoni ya wadau katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho nchini ikiwemo Mamlaka za Serikali ngazi ya Mikoa na Wilaya, Taasisi za Serikali, Vyama Vikuu vya Ushirika na Wakulima. Aidha, Sera, Mikakati na Mipango ya Taifa ilizingatiwa katika maandalizi hayo ikiwa ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa *(Tanzania Development Vision - TDV)*; Mpango wa Taswira ya Muda Mrefu wa Taifa *(Long Term Perspective Plan - LTPP)*; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano *(Third Five Year Development Plan - FYDP III 2021/22-2025/26)*; Sera ya Taifa ya Kilimo ya 2013; Sera ya Maendeleo ya Ushirika; Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(Agricultural Sector Development Program Phase II – ASDP II 2017/18 - 2027/28)*; Mkakati wa Tasnia ya Korosho Nchini 2023/2024 – 2029/2030 *(Cashewnut Industry Strategy 2023/2024 – 2029/2030)* na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2020. Aidha, Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009 *(The Cashewnut Industry Act No. 18, 2009)*, Sheria ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Na. 4 ya Mwaka 2020 imezingatiwa.

Vilevile, Mwongozo huu umezingatia mipango na programu za kikanda na kimataifa zinazohusu sekta ya kilimo ikiwemo Programu Kabambe ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Afrika *(CAADP, 2015-2025)*; Malengo ya Maendeleo Endelevu *(Sustainable Develepment Goals-SDGs)* pamoja na itifaki na mikataba mbalimbali ambayo nchi imeridhia kuhusu matumizi salama ya viuatilifu kwa afya ya wanyama, mimea na mazingira (Mkataba wa Rotterdam na Stockholm).

Pia, Mwongozo huu umezingatia vipaumbele vya Wizara ya Kilimo ambavyo ni kuongeza tija na kuweka mkazo kwenye utafiti utakaozingatia ugunduzi wa aina za mbegu bora na mbinu bora za kilimo; kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora; kuimarisha huduma za ugani; kuimarisha kilimo cha umwagiliaji; kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo; kuimarisha kilimo anga kwa ajili ya kudhibiti visumbufu; na kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji.

Hivyo, ni matumaini yetu kuwa utekelezaji wa Mwongozo huu utakuwa shirikishi na utaleta manufaa yaliyokusudiwa kwa wadau wote katika Tasnia ya Korosho hapa nchini.

Natanguliza shukrani kwa ushirikiano.

Francis Alfred
**MKURUGENZI MKUU**
Tarehe 17th April, 2025

## 1.0 UTANGULIZI

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali ngazi ya Mikoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Pamoja na Taasisi nyingine zikiwemo Umma na zile binafsi na zilizopo kwenye mnyororo wa thamani wa zao la korosho hapa nchini, wakulima na wadau wengine wanaendelea na maandalizi ya uzalishaji wa korosho msimu wa mwaka 2025/2026. Katika msimu wa mwaka 2025/2026 kama ilivyokuwa msimu wa mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kutoa ruzuku kwenye pembejeo zilizonunuliwa na Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Ushirika. Shabaha ya utoaji wa ruzuku kwenye pembejeo za korosho kwa wakulima ni kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji wa korosho. Hata hivyo ifahamike kwamba ***''Endapo itatokea pembejeo zinazotolewa kwa ruzuku kutokidhi mahitaji ya mkulima hususani mkulima mkubwa*****;** ***mkulima husika anakumbushwa kuweka akiba ya fedha kwa ajili ya kununua viuatilifu vinavyopungua sokoni''.***

## 2.0 MWENENDO WA USAMBAZAJI WA PEMBEJEO NA UZALISHAJI

Pembejeo za kilimo cha korosho hususani viuatilifu na mabomba katika zao la korosho ni muhimu ili kuwawezesha wakulima kuongeza tija na uzalishaji wa korosho ghafi nchini. Kwa misimu ya nyuma kabla ya msimu wa mwaka 2018/2019, Serikali ilitoa ruzuku ya asilimia hamsini (50%) ya pembejeo na mabomba isipokuwa msimu wa 2017/2018 ambapo pembejeo zilitolewa bila malipo kwa wakulima. Kuanzia msimu wa mwaka 2018/2019, Serikali haikutoa ruzuku na hivyo wakulima walijigharamia kwa kujipatia pembejeo na mabomba kutoka kwa wasambazaji waliokuwepo sokoni. Wakulima walinunua pembejeo hizo kwa fedha taslimu au mkopo ambao hata hivyo urejeshaji wake haukuwa wa kuridhisha. Mathalani; msimu wa 2018/2019 hadi msimu wa 2020/2021 Bodi ya Korosho Tanzania, Vyama Vikuu vya Ushirika na Mabenki walikopesha pembejeo kwa wakulima na mikopo hiyo haikuweza kurejeshwa kwa wakati.

Utaratibu wa wakulima kujigharamia pembejeo ulionekana kutoleta matokeo chanya. Hii ni kutokana na wakulima wengi kutokuwa na fedha za kununua pembejeo za kutosha kudhibiti visumbufu vya zao la korosho. Kumbukumbu zilizopo Bodi ya Korosho Tanzania zinaonesha kuwa uzalishaji wa korosho ghafi nchini ulipungua kutoka tani 313,826 msimu wa 2017/2018 hadi tani 210,787 msimu wa 2020/2021 kutokana na wakulima kushindwa kudhibiti visumbufu vya zao la korosho.

Uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Sita kurejesha mfumo wa ruzuku kwenye pembejeo na mabomba katika zao la korosho nchini kuanzia msimu wa 2021/2022 uliwezesha uzalishaji wa korosho ghafi kuongezeka kutoka tani 210,787 msimu wa 2020/2021 hadi tani 528,263.820 msimu wa 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 250.61. **Jedwali Na. 01** linaonesha mwenendo wa matumizi ya pembejeo na uzalishaji wa korosho ghafi nchini kuanzia msimu wa 2012/2013 hadi msimu wa 2024/2025.

**Jedwali Na. 01: Mwenendo wa Matumizi ya Pembejeo na Uzalishaji wa Korosho Ghafi Nchini kuanzia Msimu wa 2012/2013 hadi Msimu wa 2024/2025**

| Msimu | Viuatilifu vya Maji | Sulphur ya Unga (Tani) | Uzalishaji wa Korosho Ghafi (Tani) |
|---|---|---|---|
| 2012/2013 | 182,230 | 5,000 | 127,947 |
| 2013/2014 | 346,300 | 5,000 | 129,823 |
| 2014/2015 | 300,000 | 8,000 | 198,114 |
| 2015/2016 | 160,000 | 10,000 | 155,245 |
| 2016/2017 | 255,000 | 15,000 | 265,238 |
| 2017/2018 | 310,000 | 18,000 | 313,826 |
| 2018/2019 | 339,009 | 12,352 | 225,154 |
| 2019/2020 | 448,258 | 8,610 | 232,682 |
| 2020/2021 | 182,438 | 8,731 | 210,787 |
| 2021/2022 | 1,497,354 | 13,562 | 240,158 |
| 2022/2023 | 2,683,682 | 15,014 | 187,849 |
| 2023/2024 | 1,989,238 | 39,275 | 310,787 |
| 2024/2025 | 2,689,581 | 41,263 | 528,264 |

***NB:** Msimu wa 2024/2025 takwimu za uzalishaji wa korosho ghafi ni kwa mujibu taarifa zilizokusanywa hadi tarehe 14 Aprili, 2025.*

## 3.0 MADHUMUNI YA MWONGOZO


Madhumuni ya mwongozo huu ni kutoa maelekezo juu ya utaratibu wa usambazaji wa pembejeo na mabomba kwa wakulima wa korosho msimu wa 2025/2026 ikiwa ni pamoja na kuainisha majukumu ya kila mdau kwenye zoezi hilo.

## 4.0 MBINU ZILIZOTUMIKA KUTAYARISHA MWONGOZO

Mbinu mseto zimetumika katika kufanikisha maandalizi ya Mwongozo huu ikiwa ni pamoja na mapitio ya Mwongozo uliotumika msimu wa mwaka 2024/2025 sanjari na ushirikishaji wa taasisi za umma na zile za binafsi pamoja na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho hapa nchini zikiwemo Sekretarieti za Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Naliendele; Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA); Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC); Vyama Vikuu vya Ushirika *(Unions)* na Mradi wa Pamoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika (KCJEL). Hivyo, ni matumaini ya Serikali kuwa utekelezaji wa Mwongozo huu utakuwa shirikishi na utaleta manufaa yaliyokusudiwa kwa Tasnia ya Korosho hapa nchini.

## 5.0 MNYORORO WA USAMBAZAJI WA PEMBEJEO ZA RUZUKU ZA ZAO LA KOROSHO NCHINI

Kielelezo Na. 01 hapa chini kinaonesha mnyororo wa usambazaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho nchini hadi ngazi ya mkulima.




**Kielelezo Na. 01: Mfumo wa usambazaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho nchini hadi ngazi ya mkulima.**

Ununuzi wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho kwa ajili ya msimu wa 2025/2026 umefanywa na Mradi wa Pamoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika chini ya uratibu wa Bodi ya Korosho Tanzania. Vyama vinavyounda mradi huo ni MAMCU Ltd na TANECU Ltd kutoka Mkoa wa Mtwara, RUNALI Ltd na LMCU Ltd kutoka Mkoa wa Lindi, TAMCU Ltd kutoka Mkoa wa Ruvuma na CORECU Ltd kutoka Mkoa wa Pwani. Mradi unatekeleza shughuli zake hususani uagizaji wa pembejeo kwa kuzingatia taratibu, miongozo, kanuni na sheria zilizopo nchini chini ya usimamizi wa karibu wa CBT, TCDC, TARI Naliendele na TPHPA.

## 6.0 UDHIBITI WA UBORA WA PEMBEJEO

Udhibiti wa ubora wa pembejeo unazingatia taratibu, miongozo, kanuni na sheria zilizopo nchini. Aidha, kwa lengo la kujiridhisha na ubora wa pembejeo kabla ya kusambazwa kwa wakulima, Bodi ya Korosho Tanzania itachukua sampuli kwa kila toleo *(Batch No.)* la viuatilifu na kupeleka kupimwa TPHPA. Ni pembejeo zitakazokidhi viwango stahiki vya ubora tu ndizo zitakazosambazwa kwa wakulima na zile zitakazokuwa chini ya kiwango hazitasambazwa kwa wakulima na badala yake zitarejeshwa kwa wazabuni husika mwishoni mwa msimu ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Sambamba na hilo, Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele na Halmashauri kupitia maafisa kilimo wa BBT Korosho na maafisa ugani wa Kata itateua shamba la mfano kwa kila kijiji litakalotumika kama shamba darasa. Mashamba ya

mfano yatatumia pembejeo za ruzuku zinazosambazwa kwa wakulima katika msimu wa 2025/2026 kwa ajili ya kuonesha kwa vitendo juu ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu.

## 7.0 GHALA KUU ZA PEMBEJEO

Ili kupunguza gharama za usafirishaji kutoka ghala kuu kwenda kwa wakulima, ghala kuu zimeandaliwa kwenye Mkoa wa Mtwara ambapo zitakuwa katika Halmashauri za Mtwara Mikindani, Tandahimba na Masasi Mji; Mkoa wa Lindi zitakuwa kwenye Manispaa ya Lindi; Mkoa wa Pwani zitakuwa Halmashauri ya Kibiti na Mkoa wa Ruvuma zitakuwa katika Halmashauri ya Tunduru. Ghala Kuu zote zitakuwa chini ya uendeshaji wa Meneja Dhamana aliyepewa kazi hiyo na KCJEL chini ya uratibu na usimamizi wa CBT.

Ghala Kuu za Mtwara Mikindani, Tandahimba na Masasi Mji zitapokea na kuhifadhi pembejeo za Mkoa wa Mtwara; Ghala Kuu la Manispaa ya Lindi litapokea na kuhifadhi pembejeo za Mkoa wa Lindi; Ghala Kuu la Tunduru Mjini litapokea na kuhifadhi pembejeo za Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Mbeya na Songwe; na Ghala Kuu la Kibiti Mjini litapokea na kuhifadhi pembejeo za Mikoa ya Pwani, Tanga na mikoa mipya iliyobakia.

## 8.0 USAFIRISHAJI WA PEMBEJEO

Wazabuni wa pembejeo watasafirisha pembejeo hadi kwenye ghala kuu kadri watakavyoelekezwa na KCJE Ltd kwa kushirikiana na CBT. Jukumu la kusafirisha pembejeo kutoka ghala kuu kwenda AMCOS kwa mikoa ya asili na mikoa mipya litakuwa chini ya KCJEL kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika na CBT.

## 9.0 MFUMO WA KIDIJITALI WA UGAWAJI WA PEMBEJEO

Mfumo utakaotumika kugawa viuatilifu kwa wakulima msimu wa 2025/2026 ni Mfumo wa Usambazaji wa Pembejeo za Kilimo *(Agriculture Input Subsidy System - AISS)* uliopo Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA). Kupitia mfumo huo, wadau muhimu wakiwemo wakulima, maafisa kilimo wa BBT Korosho, AMCOS, Vyama Vikuu vya Ushirika, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri na CBT watasajiliwa. Aidha, mfumo huo utaratibu usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima kupitia *QR code* za kielektroniki.

## 10.0 USAJILI WA VITUO VYA KUGAWA PEMBEJEO

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri na Vyama Vikuu vya Ushirika itasajili AMCOS zitakazotumika kupokea na kugawa pembejeo kwa wakulima. AMCOS hizo ni zile zenye ghala zinazokidhi viwango na pia miundombinu ya barabara inayofikika kwa urahisi pamoja na upatikanaji wa mtandao wa *internet*. Aidha, ili kuwa na ufanisi katika zoezi la usambazaji na ugawaji wa viuatilifu kwa wakulima; AMCOS zinashauriwa kutenga ghala maalum kwa ajili ya kupokea na kugawa viuatilifu tofauti na yale yanayotumika kwenye ukusanyaji na uuzaji wa mazao ya ufuta na mbaazi.

### 10.1. UTARATIBU WA UGAWAJI WA PEMBEJEO

### 10.2. Usajili/Uhuishaji wa Kanzidata ya Wakulima wa Korosho

Ugawaji wa pembejeo kwa wakulima utafanyika kwa wale watakaokuwa wamehuisha taarifa zao au kusajiliwa (Endapo ni mkulima mpya) msimu wa 2025/2026 kupitia njia mojawapo kati ya hizi zifuatazo:-

i. Mfumo wa AISS kupitia *CBT Tool App*. *App* hiyo itakuwa na taarifa muhimu ikiwemo idadi wa mikorosho, ukubwa wa shamba na picha ya mkulima na hatimaye kutoa namba ya mkulima *(Farmer Identification Number – Farmer ID)* itakayotumika kumtambua mkulima atakayepokea pembejeo kupitia Neno Siri la Maramoja *(One Time Password (OTP))*; na
ii. Kupitia Kitabu/Daftari Maalumu la Usajili kwa Wakulima kwa Mikoa ambayo haijafikiwa na zoezi la usajili kwa kutumia mfumo kidijitali.

***MUHIMU: Namba ya Mkulima pamoja na OTP itatumika kama utambulisho wa mkulima wakati wa kupata huduma ya pembejeo za ruzuku za korosho msimu wa mwaka 2025/2026.***

### 10.3. Mgao na Ugawaji wa Pembejeo kwa Wakulima

Mgao wa pembejeo za ruzuku hususani viuatilifu utazingatia takwimu za usajili wa wakulima ambazo ni idadi ya miti ya mikorosho iliyohuishwa kwenye kanzidata. Hata hivyo, kutokana na mahitaji halisi ya pembejeo kwa wakulima kutoendana na mpango wa ruzuku wa Serikali, uwiano kutoka kwenye takwimu hizo utatumika kuandaa mgao halisi wa viuatilifu kwa mkulima mmoja mmoja kwa kuzingatia idadi ya mikorosho kama ilivyotajwa hapo juu.

***Kwa mantiki hiyo, wakulima wanakumbushwa kwamba ruzuku inayotolewa na Serikali ni mchango katika kumpunguzia mkulima gharama za kuzalisha korosho nchini. Kila mkulima anapaswa kuweka akiba ya fedha kwa ajili ya shughuli za maandalizi ya shamba la mikorosho ikiwemo kununua viuatilifu sokoni vya kutosheleza mahitaji yake halisi***.

Kwa upande wa utaratibu wa ugawaji, mkulima atatakiwa kwenda kwenye AMCOS iliyopo ndani ya kata anapoishi kwa ajili ya kupokea mgao akiwa na **Namba ya Utambulisho wa Mkulima *(Farmer Identification Number – Farmer ID)*** pamoja na **Kitambulisho cha Mpiga Kura** au **Kitambulisho cha Utaifa (NIDA) au Leseni ya Udereva** kwa ajili ya uhakiki wa taarifa za mkulima kabla ya kukabidhiwa mgao wake. Kwa wakulima wasio na kitambulisho watatakiwa kupata barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji/Mtaa anaoishi kwa ajili ya kumtambulisha ili aweze kupatiwa huduma ya pembejeo. Inasisitizwa mkulima kufika mwenyewe kuchukua mgao wake wa viuatilifu. Hivyo hairuhusiwi mkulima kumchukulia mkulima mwenzake mgawo wa viuatilifu.

Mgawaji wa viuatilifu katika AMCOS chini ya usimamizi wa afisa kilimo wa BBT Korosho na afisa ugani wa kata; atatakiwa kuhakiki namba ya mkulima kabla ya kumpatia huduma na baada ya kujiridhisha kuwa taarifa zake zinaendana na zile zilizopo kwenye kitambulisho cha NIDA au Mpiga Kura au Barua ya Utambulisho kutoka Ofisi ya Kijiji/Mtaa. Kisha ataingiza namba ya mkulima kwenye mfumo na mkulima atapata ujumbe mfupi papo hapo (*One Time Password – OTP*) ukimtaka kuweka nywila au neno

la siri kwenye simu yake ili kukiri na kukamilisha taratibu za kupata mgao wake. Kwa mkulima ambaye namba yake ya simu itakuwa imekosewa atatakiwa kumweleza Afisa kilimo wa BBT korosho kwa ajili ya kurekebisha taarifa zake kwenye mfumo.

***MUHIMU: Ikumbukwe kuwa mkulima asiye na namba ya simu (Line) hataweza kupata mgao wake wa pembejeo.***

## 11.0 JINSI USAMBAZAJI NA UGAWAJI WA PEMBEJEO ULIVYO

Usambazaji na ugawaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho kwa mfumo wa kidijitali katika msimu wa mwaka 2025/2026 utazingatia utaratibu ufuatao: -

i. Wazabuni wataingiza pembejeo nchini kwa mujibu wa mikataba baina yao na KCJE Ltd. Pembejeo hizo zitawasilishwa kwenye ghala kuu zilizopo mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma ambazo zipo chini ya usimamizi wa Meneja Dhamana wa Kampuni ya *ACE Global Depository (Tanzania) Ltd*;
ii. Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika na Halmashauri husika zitasajili AMCOS za ugawaji wa pembejeo kwa wakulima;
iii. Wakulima watasajiliwa kwenye kanzidata ya kielektroniki na kupatiwa namba za utambulisho ambazo watazitumia kupata huduma ya pembejeo kwenye ghala za AMCOS;
iv. Mradi wa Pamoja kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika vitasafirisha pembejeo kutoka ghala kuu kwenda AMCOS;
v. AMCOS chini ya usimamizi wa Afisa Kilimo wa BBT Korosho na Afisa Ugani wa Kata watatumia mfumo wa kidijitali kugawa viuatilifu kwa wakulima; na
vi. Kwa upande wa mabomba, hayatasambazwa kwa njia ya mfumo wa ugawaji pembejeo isipokuwa kwa mkulima atakayehitaji bomba la kupulizia atatakiwa kuchangia nusu ya gharama kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 3** hapo chini.

**Jedwali Na. 3: Bei ya soko ya bomba na nusu yake ambayo mkulima anatakiwa kuchangia.**

| Na. | Chapa ya Bomba | Bei ya Soko (Tshs.) | Nusu ya Bei ya Soko (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1 | *Pulmic take control* | 1,195,000.00 | 597,500.00 |

## 12.0 UTOAJI WA ADHABU

Utekelezaji wa Mwongozo huu utazingatia sheria za Tanzania ikiwemo Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009 na Kanuni zake za Mwaka 2010. Wadau wote wanapaswa kuzingatia Sheria za nchi ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Mwongozo huu. Vitendo vyovyote vya ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu au vitakavyobainika kuwa na lengo la kukwamisha utaratibu wa ugawaji wa pembejeo kwa mtu yeyote hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

## 13.0 USIMAMIZI, UFUATILIAJI NA TATHMINI

Jukumu la kusimamia na kufuatilia mwenendo wa zoezi zima la usambazaji wa pembejeo ni la ngazi zote kuanzia Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, CBT, TCDC, TARI, TPHPA, Vyama Vikuu vya Ushirika na AMCOS. Ili kuwa na ufanisi wa usambazaji wa pembejeo kila Mkoa na Halmashauri zake zitaunda **Kikosi Kazi**

*(**Task Force**)* cha kusimamia na kufuatilia mwenendo wa mapokezi na usambazaji wa pembejeo katika eneo lake. Vikosi Kazi vitakavyoundwa vitakuwa kama ifuatavyo:-

### 13.1. Muundo wa Kikosi Kazi Mkoa
Kitaundwa na Wajumbe wa Kamati ya Pembejeo ya Mkoa.

### 13.2. Muundo wa Kikosi Kazi Wilaya
Kitaundwa na Wajumbe wa Kamati ya Pembejeo ya Wilaya.

### 13.3. Muundo wa Kikosi Kazi Kata
Kitaundwa na Wajumbe wa Kamati ya Pembejeo ya Kata.

### 13.4. Sekretarieti ya Ugawaji wa Pembejeo ngazi ya AMCOS
Itaundwa na Afisa Kilimo Kata/Kijiji/Mtaa, Afisa Kilimo BBT Korosho, Katibu wa AMCOS na Mwenyekiti wa Kijiji husika.

## 14.0 UGHARAMIAJI WA VIKOSI KAZI
Kwa kuwa vikosi kazi katika ngazi mbalimbali vitakuwa chini ya taasisi ambazo ni wanufaika wa zao la korosho; inashauriwa ugharamiaji ufanywe na taasisi hizo.

## 15.0 GHARAMA ZA USAFIRISHAJI WA PEMBEJEO
Shughuli ya usafirishaji wa pembejeo kutoka ghala kuu kwenda AMCOS ikiwa ni pamoja na upakiaji na ushushaji gharama zitalipwa na KCJEL Ltd. Kwa upande wa shughuli ya ulinzi na usalama wa viuatilifu baada ya kupokelewa katika ghala za AMCOS litakuwa chini ya AMCOS husika. Ugawaji wa viuatilifu kwa wakulima utafanywa na AMCOS chini ya usimamizi wa Afisa Kilimo wa BBT Korosho, Afisa Ugani wa Kata/Kijiji/Mtaa na Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa husika.

## 16.0 UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO
Endapo kutatokea malalamiko yoyote juu ya usambazaji na ugawaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho yatawasilishwa na kushughulikiwa kulingana na ngazi za utekelezaji kuanzia Ofisi ya Kijiji/Mtaa/Kata, AMCOS, Halmashauri, Chama Kikuu cha Ushirika, Wilaya, Mkoa na Bodi ya Korosho Tanzania.

Ili kurahisisha mawasiliano, Bodi ya Korosho Tanzania ina namba ya simu ya bure ambayo ni ***0 8 0 0 1 1 2 1 5 9*** kwa ajili ya kupokea maoni, ushauri, malalamiko na kuyashughulikia kulingana na ngazi husika.

## 17.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU
Ili kuhakikisha zoezi la ugawaji wa pembejeo linakuwa na ufanisi kutakuwa na mgawanyo wa majukumu ya kiutendaji na kitaasisi kama inavyoonekana hapa chini:-

### 17.1. Wizara ya Kilimo
(i) Kutoa na kusimamia miongozo ya kisera juu ya ununuzi na usambazaji wa pembejeo, mabomba na magunia katika zao la korosho;
(ii) Kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kulipia gharama ya pembejeo zitakazosambazwa kwa wakulima; na
(iii) Kushughulikia masuala mengine yatakayohitaji maamuzi ya Wizara juu ya pembejeo za ruzuku za zao la korosho.

### 17.2. Kikosi Kazi cha Mkoa

(i) Kuandaa mpango wa ufuatiliaji wa usambazaji wa pembejeo ndani ya mkoa wake;
(ii) Kuratibu mgao wa pembejeo za zao la korosho kwenye Halmashauri ndani ya Mkoa;
(iii) Kushirikiana na CBT, TPHPA, TARI Naliendele, TCDC na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(iv) Kuratibu shughuli za kikosi kazi cha Mkoa kwenye usimamizi na ufuatiliaji wa zoezi la usambazaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho;
(v) Kuchukua hatua za kisheria kwa mtu yeyote atakayebainika kukiuka utaratibu wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo;
(vi) Kuhakikisha uwepo wa vituo vya kugawa pembejeo kwa wakulima kupitia AMCOS;
(vii) Kutoa maelekezo kwa wadau yanaolenga kuboresha mwenendo wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima ndani ya Mkoa; na
(viii) Kusimamia na kuhakikisha zinatengwa ghala za AMCOS/Vijiji kwa ajili ya kupokelea mazao ya ufuta na mbaazi ambazo hazitatumika kupokea na kugawa viuatilifu kwa wakulima.

### 17.3. Kikosi Kazi cha Wilaya

(i) Kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika husika kupokea migao ya pembejeo ghala kuu na kuipeleka kwenye maeneo husika;
(ii) Kuandaa mpango wa ufuatiliaji wa mapokezi na usambazaji wa pembejeo ndani ya Wilaya;
(iii) Kufuatilia migao ya viuatilifu ghala kuu na kutengeneza migawo kwa kila AMCOS zilizo ndani ya Kata na Halmashauri husika;
(iv) Kushirikiana na CBT, TPHPA, TARI Naliendele, TCDC na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(v) Kuchukua hatua za kisheria kwa mtu yeyote atakayebainika kukiuka utaratibu wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo;
(vi) Kusimamia na kuhakikisha zinatengwa ghala za AMCOS/Vijiji kwa ajili ya kupokelea mazao ya ufuta na mbaazi ambazo hazitatumika kupokea na kugawa viuatilifu kwa wakulima;
(vii) Kushirikiana na CBT kuwasimamia Maafisa Kilimo wa BBT Korosho katika usajili, usambazaji/ugawaji wa pembejeo pamoja na utekelezaji wa majukumu mengine ya tasnia ya korosho;
(viii) Kutatua changamoto za usambazaji wa pembejeo kadiri zinavyojitokeza.

### 17.4. Kikosi Kazi cha Kata

(i) Kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika husika kupokea pembejeo zinazowasili na kukiri mapokezi yake;
(ii) Kuandaa ratiba ya ugawaji wa viuatilifu kwa wakulima ndani ya Kata;
(iii) Kuratibu mapokezi ya pembejeo za zao la korosho zinazopokelewa ndani ya kata husika;
(iv) Kuhamasisha wakulima kujitokeza kwenye mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu pale yatolewapo;

(v) Kutoa elimu ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu vinavyowasilishwa kabla ya kusambazwa kwa wakulima;
(vi) Kugawa pembejeo kwa wakulima waliosajiliwa kwenye mfumo tu;
(vii) Kuzuia na kutoa taarifa ya wakulima wenye migawo mikubwa tofauti na uhalisia kabla ya kuitoa kwenye mfumo;
(viii) Kufuatilia na kusimamia katika kuhakikisha kuwa Maafisa Kilimo Kata, Maafisa Kilimo wa BBT Korosho na Viongozi wa AMCOS wanashiriki kikamilifu katika usambazaji/ugawaji wa pembejeo kwa wakulima; na
(ix) Kutatua changamoto za usambazaji wa pembejeo kadiri zinavyojitokeza.

**17.5. Sekretarieti ya Ugawaji wa Pembejeo Kata**

(i) Itaundwa na Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa, Mtendaji wa Kijiji/Mtaa, Katibu wa AMCOS, Afisa Kilimo Kata/Kijiji/Mtaa; na Afisa Kilimo wa BBT (kwa Maeneo ambayo wapo);
(ii) Kuhakiki taarifa za wakulima kabla ya kupata huduma ya pembejeo
(iii) Kugawa pembejeo kwa wakulima wenye sifa na kutatua changamoto za ugawaji wa pembejeo;
(iv) Kutoa elimu ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kabla kuanza kugawa viuatilifu kwa wakulima;
(v) Kumuonesha mkulima mgawo wake kwa ajili ya kujiridhisha kabla ya kugawiwa;
(vi) Katibu wa AMCOS atakuwa na mfumo wa kusambaza pembejeo kwa wakulima;
(vii) Kuhakiki, kurekebisha, kusajili na kuhuisha taarifa ya mkulima ambaye watajiridhisha pasina shaka kuwa ni mkulima halali ili aweze kupata huduma ya pembejeo;
(viii) Kuandaa ratiba ya usambazaji pembejeo kwa wakulima na kuibandika kwenye mbao za matangazo; na
(ix) Kuwahudumia wakulima pasipo upendeleo wala ubaguzi kutokana na hali na kipato cha mkulima.

**17.6. Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania**

(i) Kutoa waraka unaoainisha wajibu wa Vyama vya Ushirika husika kutekeleza maelekezo ya Serikali juu ya uagizaji na usambazaji wa pembejeo na mabomba kwa wakulima msimu wa 2025/2026;
(ii) Kuvielekeza vyama vikuu vya ushirika kuwawezesha Makatibu wa AMCOS kushiriki kwenye mafunzo ya mfumo wa usambazaji wa pembejeo, kusimamia ugawaji wa pembejeo na ulinzi wa pembejeo ziwapo kwenye vituo vya kugawa pembejeo;
(iii) Kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya pembejeo, na magunia iliyofungwa kati ya wazabuni na KCJEL;
(iv) Kushirikiana na CBT, Sekretarieti ya Pembejeo, TPHPA, TARI Naliendele, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(v) Kutoa maelekezo na kuchukua hatua stahiki kwa watendani na viongozi wa ushirika wanaokiuka utaratibu wa upatikanaji, usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima taratibu; na

(vi) Kufuatilia na kusimamamia mwenendo wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo kutoka vyama vya ushirika kwenda kwa wakulima.

**17.7. Bodi ya Korosho Tanzania**

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia mpango wa ruzuku ya pembejeo za zao la korosho;
(ii) Kuhuisha na kusajili wakulima wa zao la korosho nchini;
(iii) Kushirikiana na Vikosi Kazi katika ngazi mbalimbali kwenye usimamizi wa mapokezi, usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima;
(iv) Kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya pembejeo, mabomba na magunia iliyofungwa kati ya wazabuni na KCJEL;
(v) Kuhakikisha pembejeo, mabomba na magunia yanasambazwa kwa wakulima kwa kuzingatia taratibu;
(vi) Kufuatilia, kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza taarifa zinazohusu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za zao la korosho;
(vii) Kupokea nakala za mikataba yote iliyoingiwa na wazabuni kwa ajili ya kuingiza na kusambaza pembejeo kwa wakulima toka KCJE Ltd;
(viii) Kupokea nakala za Hati za kuleta pembejeo toka kwa Wazabuni na Hati ya Kukiri Kupokea *(Delivery Note and Good Received Note)*, Hati ya Usambazaji kwenda Vyama Vikuu *(Delivery Note)* na Hati za Madai ya wazabuni *(Invoice);*
(ix) Kuratibu mafunzo ya mfumo wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa AMCOS zilizoteuliwa kutekeleza shughuli hiyo;
(x) Kushirikiana na TPHPA, TARI Naliendele, TCDC, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(xi) Kusimamia utekelezaji wa mwongozo huu katika ngazi zote na kuchukua hatua za kiutendaji;
(xii) Kushirikiana na Halmashauri kusimamia Maafisa Kilimo wa BBT Korosho katika usajili na usambazaji/ugawaji wa viuatilifu kwa wakulima;
(xiii) Kuandaa rasimu ya mwongozo wa upatikanaji, usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima na kuitisha kikao rasmi kwa ajili ya kuijadili na kupitisha mwongozo kwa ajili ya utekelezaji;
(xiv) Kutengeneza akaunti ya kila Mkoa na Halmashauri kwa ajili ya kuona mwenendo wa usajili wa wakulima na usambazaji wa pembejeo; na
(xv) Kulipia gharama zinazotokana na uhudumiaji wa mfumo wa AISS ikiwa ni pamoja na maboresho yake kwa TFRA.

**17.8. Vyama Vikuu vya Ushirika**

(i) Kufanya manunuzi ya pembejeo, mabomba na magunia kupitia Mradi wa Pamoja wa Ushirika wa Korosho - KCJE kwa kuzingatia taratibu, miongozo, kanuni na sheria zilizopo;
(ii) Kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(iii) Kuandaa ghala za kupokelea pembejeo, mabomba na magunia kutoka ghala kuu kwenda kwa wakulima;
(iv) Kupokea pembejeo, mabomba na magunia kutoka kwa wazabuni;

(v) Kushirikiana na KCJEL kusafirisha pembejeo, mabomba na magunia kutoka ghala kuu kwenda vituo vya ugawaji;
(vi) Kusimamia usambazaji na ugawaji wa pembejeo, mabomba na magunia katika eneo husika; na
(vii) Kupitia na kuhakiki nyaraka/ankara za madai kwa lengo la kujiridhisha na usahihi wake kabla ya kuwalipa wazabuni.

**17.9. Vyama vya Ushirika vya Msingi - AMCOS**

(i) Kusajili ghala litakalotumika kupokea na kugawa pembejeo;
(ii) Kuhakiki, kupokea na kutunza pembejeo za wakulima;
(iii) Kushirikiana na Afisa Kilimo Kata/Kijiji/Mtaa, Afisa Kilimo wa BBT Korosho na Mwenyekiti wa Kijiji husika katika ugawaji wa pembejeo kwa wakulima;
(iv) Kupokea mafunzo ya mfumo wa ugawaji wa pembejeo na mabomba;
(v) Kushirikiana na Kikosi Kazi Kata kupokea pembejeo na kugawa kwa wakulima kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa;
(vi) Kuandaa mabango ya wakulima walionufaika na mgawo wa pembejeo na kubandika kwenye bao za matangazo;

**17.10. TARI Naliendele**

(i) Kuthibitisha endapo kiuatilifu kimefanyiwa majaribio kwenye zao la korosho;
(ii) Kutoa viwango vya uzimuaji wa viuatilifu kwa viuatilifu vilivyopo kwenye mpango kwa msimu wa mwaka 2025;
(iii) Kushirikiana na Bodi ya Korosho, TCDC, TPHPA, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu na kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(iv) Kufuatilia mwenendo wa uzalishaji wa korosho na hali ya hewa na kutoa ushauri wa kitaalam juu matumizi ya viuatilifu;
(v) Kutoa mapendekezo ya pembejeo na mabomba yanayofaa kuagizwa na kusambazwa kwa wakulima; na
(vi) Kushirikiana na CBT, TPHPA kuendesha mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima.

**17.11. Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania – TFRA**

i. Kutoa huduma ya Mfumo wa Usajili wa Wakulima na Usambazaji wa Pembejeo;
ii. Kufanya maboresho ya Mfumo kulingana na mahitaji ya usajili na usambazaji wa pembejeo za korosho;
iii. Kuwasilisha Bodi ya Korosho Tanzania barua ya gharama za uhudumiaji wa mfumo na matengenezo

**17.12. KCJEL Ltd**

(i) Kulipa wazabuni na watoa huduma wengine kwa kuzingatia mikataba;
(ii) Kusaini mikataba na wazabuni wa usambazaji wa pembejeo, mabomba na magunia;
(iii) Kusimamia utekelezaji wa mikataba ulioingiwa na wazabuni;
(iv) Kuandaa ghala kuu za mapokezi ya pembejeo, mabomba na magunia kutoka kwa wazabuni kabla ya kusambazwa kwenda kwa wakulima;
(v) Kutafuta ghala za kuhifadhi pembejeo, kulipa washushaji na wapakiaji pamoja na wasafirishaji kutoka ghala kuu kwenda ghala za AMCOS;

(vi) Kutoa viwango vya usafirishaji wa viuatilifu kwa vyama vikuu kwa ajili ya kuingiwa na wasafirishaji pale itakapo hitajika kufanya hivyo ili kunusuru hali;
(vii) Kutafuta na kuingia mikataba na wasafirishaji wa pembejeo kutoka ghala kuu kwenda ghala za AMCOS kwa ajili ya kusambazwa
(viii) Kuwasilisha Bodi ya Korosho Tanzania nakala za mikataba yote iliyoingiwa na wazabuni kwa ajili ya kuingiza na kusambaza pembejeo kwa wakulima;
(ix) Kuwasilisha Bodi ya Korosho nakala za Hati za kuleta pembejeo toka kwa Wazabuni na Hati ya Kukiri Kupokea (Delbery Note and Good Received Note); Hati Usambazaji kwenda Vyama Vikuu (Delivery Note) na Hati za Madai ya wazabuni – Invoice.

### 17.13. Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania

(i) Kuainisha viambata amilifu *(Active ingredients)* kwenye viuatilifu vya zao la korosho kwa lengo la kulinda viwango na ubora;
(ii) Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania, TCDC, TARI Naliendele, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa maafisa ugani, wapuliziaji na wakulima;
(iii) Kufanya ukaguzi mara kwa mara wa viuatilifu vya korosho vinavyotumika nchini na kuchukua hatua pale sheria husika inapokiukwa;
(iv) Kujiridhisha na ubora wa viuatilifu vyote kabla ya kusambaza kwa wakulima.

### 17.14. Wazabuni wa Pembejeo

i. Kuagiza na kusambaza pembejeo kwa mujibu wa mkataba baina yake na KCJEL;
ii. Kuingiza Viuatilifu vinavyokidhi viwango vya ubora kwa kuzingatia mwongozo, sheria na matakwa ya mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA).
iii. Kuwasilisha KCJEL nyaraka za idhini ya kuingiza viuatilifu nchini na matokeo ya ubora wa viuatilifu alivyoagiza toka TPHPA kabla ya kupokelewa na kusambazwa kwa mujibu wa Mwongozo huu;
iv. Kuwasilisha hati za madai kwa mujibu wa mkataba; na
v. Kujiepusha na vitendo vya udanganyifu na ukiukwaji wa sheria na Mwongozo huu.

### 17.15. Mkulima wa Zao la Korosho

i. Kuhakikisha kuwa amesajiliwa na amehuisha taarifa zake kwenye kanzidata ya wakulima wa korosho iliyopo Bodi ya Korosho Tanzania;
ii. Kuhakikisha kuwa shamba lake ni safi;
iii. Kutumia pembejeo kwa usahihi, yaani kutimiza idadi ya mipulizo inayotakiwa na kutumia viwango na vipimo sahihi kama inavyoelekezwa na mtaalam wa kilimo (Afisa Kilimo) aliyepo katika eneo lake;
iv. Kutunza kumbukumbu za matumizi ya pembejeo kwa kuandika kwenye daftari na kutunza nyaraka za mapokezi ya viuatilifu kutoka kwa mgawaji;
v. Hairuhusiwi kutumia namba ya mkulima zaidi ya moja kupata huduma za pembejeo;
vi. Haruhusiwi kuuza wala kununua pembejeo za bure zinazotolewa na Serikali;
vii. Kutoa taarifa kwa Afisa Kilimo juu ya ukiukwaji wowote wa Mwongozo;

**17.16. Taasisi za Fedha**

i. Kutoa huduma za kifedha kwa wadau wa korosho nchini ikiwa ni pamoja na wakulima na wazabuni wa pembejeo; na
ii. Kutoa elimu ya huduma za kifedha kwa wadau wa korosho ikiwa ni pamoja na wakulima na wazabuni wa pembejeo.

**17.17. Waandishi wa Habari**

i. Kuhabarisha umma juu ya taarifa za upatikanaji, usambazaji, ugawaji na matumizi ya pembejeo za korosho.
ii. Kutoa taarifa sahihi za utekelezaji wa mwongozo huu

## 18.0 WAJIBU WA PAMOJA

i. Kuhakikisha majukumu haya yanatekelezwa kwa kuzingatia sera na sheria za nchi;
ii. Kutoa taarifa mapema kuhusu suala lolote ambalo litakwamisha utekelezaji wa mpango huu.
iii. Kuhakikisha pembejeo zinamnufaisha mkulima akiwa mtumiaji wa mwisho na sio mtu wa kati au asiye mlengwa wa utaratibu wa ugawaji pembejeo za ruzuku.
iv. Kuhakikisha kila mdau husika anatimiza wajibu wake.

## 19.0 MUDA WA UTEKELEZAJI

Mwongozo huu utatekelezwa kipindi chote cha mapokezi na usambazaji wa pembejeo za msimu wa 2025/2026.

## 20.0 ILANI

Serikali haitawajibika kwa namna yoyote ile kwa mdau ambaye hatazingatia utaratibu uliowekwa kwenye Mwongozo huu.

## 21.0 HITIMISHO

Serikali imeamua kuendelea kutoa ruzuku ya pembejeo za korosho kwa wakulima wa zao la korosho nchini ili waweze kuongeza tija na uzalishaji wa korosho ghafi. Hii ni kutokana na mchango mkubwa wa zao la korosho kwenye pato la mkulima na Taifa kwa ujumla. Hivyo basi, ni wajibu wa wadau wote wanaohusika kutekeleza majukumu yao kikamilifu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Serikali inahimiza ushirikiano wa wadau katika ngazi zote ili kuhakikisha kuwa mpango huu wa ruzuku unatekelezwa kwa ufanisi. Mwisho ingawa siyo kwa umuhimu, Mwongozo huu unaweza kufanyiwa maboresho wakati wowote kulingana na mahitaji kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa mpango wa ruzuku.

Mwongozo huu umetolewa na kusainiwa leo tarehe **17th Aprili, 2024**

Francis Alfred
**Mkurugenzi Mkuu**
Bodi ya Korosho Tanzania